

ANGALIA SANA

1. Ati kwamba umahiri, wa sharia musfadi,
Na alimu na amiri, kwa kila jambo jadidi,
Kwa baya sana mandhari, na kujenga ukaidi,
Si mtu, apenda tadi, ni mtu mwenye hatari.
2. Mahibuye na dhamiri, kutoa hiyo baridi,
Ili uwe penye hari, tangu sasa hadi hadi,
Kun na kun johari, watakaje ustadi!
Si mtu, apenda tadi, ni mtu mwenye hatari.
3. Kukandamiza uzuri, unawili ukaidi,
Ili iwepo hatari, apendako yajimidi,
Hafai japo kwa mari, si uledi si uledi,
Si mtu, apenda tadi, ni mtu mwenye hatari.
4. Kujitia ushairi na kukashifu madadi,
Aona kwake fahari kwani kaisha jifidi,
Ili hali ni kiburi, si mzia maridadi,
Si mtu, apenda tadi, ni mtu mwenye hatari.
5. Ni muovu na dahiri, wengi wameniradidi,
Mburugaji uturi, pomboo litie tadi,
Insha Allahu Qahari, yasizunguke zabadi,
Si mtu, apenda tadi, ni mtu mwenye hatari.
6. Utakapo tenda zuri, yeye apenda kuhidi,
Ataka usiwe shwari, na kuzuia juhudi,
Na kutoa machachari, huonakwe maridadi,
Si mtu, apenda tadi, ni mtu mwenye hatari.
7. Nimebuga kijasiri, hadi kujua fuadi,
Itendavyo ki dahari, kuwatenzi tilmidi,
Ela kuiuza heri, na kujinadi jinadi,
Si mtu, apenda tadi, ni mtu mwenye hatari.
8. Naona yanakithiri, Aga ninayo radidi,
Sasa yafaa saburi, mengine nisiyanadi,
Mdaawa akasiri, na kunivunja mradi,
Si mtu, apenda tadi, ni mtu mwenye hatari.

Hamidu R. Tambwe